




Ni nani Mtume Muhammad ﷺ, na kitu gani
ametufundisha?



Ameweka taaliki Sheikh Duktur Haytham Sarhaan

Mwalim wa zamani masjid annabawiy

Na msimamizi wa maahad ya sunna.



Au pangusa bar code - sarhaan.com

Muhammad

Ni nani Mtume Muhammad ﷺ
na kitu gani ametufundisha?

- Yeye ndio ametetea haki zote za viumbe tangu miaka 1400 ilopita.
- Amehifadhi haki za wanaume, wanawake, watoto na wanyonge.
- Amehifadhi haki za wanyama mimea na akahimiza kutunza mazingira.
- Ametuamrisha tabia njema na akapangilia mahusiano baina ya ndugu wa karibu na majirani.
- Na (akaasisi uhusiano) ya kuishi baina ya waislam na wasiokuwa waislam.
- Na akapangilia mahusiano ya kifamilia ambayo yanahifadhi haki kubwa za baba na mama kwa watoto wao.

Muhammad

Ni nani Mtume Muhammad ﷺ
na kitu gani ametufundisha?

- Amekataza dhulma na akalingania katika uadilifu na mapenzi na kushikamana na kusaidiana katika kheri.
- Amelingania katika kusaidia wenye kuhitaji na kutembelea wagonjwa na kupendana na kunasihiana baina ya watu wote.
- Amekataza waislamu matendo maovu kama wizi na ghishi na uuwaji na dhulma.
- Yeye ndo amebadilisha maisha yetu na tabia zetu mbaya kuja katika (tabia) nzuri.
- (Amemfundisha) musulam asiibe.
- (Amemfundisha) muislam asidanganye.
- (Amemfundisha) muislam asinywe pombe.

Muhammad

Ni nani Mtume Muhammad ﷺ
na kitu gani ametufundisha?

- Amemfundisha muislam asizini.
- Amemfundisha muislamu asifanye ghishi.
- (Amemfundisha) musilam asiue wasiokuwa na hatia.
- Amemfundisha muislam asimuudhi jirani yake awe muislam au kafiri.
- Amemfundisha muislam kuwafanyia wema wazazi wake na awa-hudumie hata kama watakuwa si katika dini yake.
- Amemfundisha muislam kuwaonea huruma watoto na wanawake na wanyonge na watu wazima.
- Amemfundisha muislam asiadhibu watu wala wanyama wala asihari-bu mazingira.

Muhammad

Ni nani Mtume Muhammad ﷺ
na kitu gani ametufundisha?

- Amemfundisha muislam amuhurumie na kumpenda mke wake na awatilie umuhimu na kuwaonea huruma watoto zake mpaka siku ya mwisho ya umri wake.
- Amemfundisha muislam asikate mahusiano na watoto wake kwa kufikia watoto wake umri wa balehe.
- Kila muislamu anampenda Muhammad ﷺ kuliko viumbe vyote.
- Amebashir ujio wake Musa na Issa juu yao amani.
- Kila muislam (anampenda) musa na isa na anaamini ya kwamba wao ni katika mitume bora juu yao amani.
- Ametumwa Muhammad ﷺ kwa waarabu na wasio kuwa waarabu.

Muhammad

Ni nani Mtume Muhammad ﷺ
na kitu gani ametufundisha?

- Na hakuna tofauti katika dini yake baina ya mwarabu na asiekuwa mwarabu isipokuwa kwa uchamungu.
- Hakika yeye ni Muhammad ﷺ mtume wa Allah .
- Je mmetambua kwa kwa nini waislamu wote wanampenda Muhammad ﷺ?
- (Je mumejua Muhammad ni nani kwa waislamu?)

Kwa ziada ya elimu kuhusu Mtume Muhammad ﷺ na mafunzo yake...



Website ya sheikh



sarhaan.com



Maahad ya sunna



mahadsunnah.com